## Orodha ya hospitali na vituo vya afya vinavyotoa huduma ya bure ya Tohara kwa wanaume

**VITUO VYA TABORA**

- Hospitali ya Mkoa - Kitete
- Hospitali ya Wilaya - Nzega
- Hospitali ya Wilaya - Igunga
- Hospitali ya Nkinga
- Hospitali ya Wilaya - Urambo
- Kituo cha Afya Kaliua

**VITUO VYA IRINGA**

- Kituo cha Afya Ngome
- Hospitali ya Mkoa Iringa
- Hospitali ya Tosamaganga (DDH)
- Hospitali ya Ilula(DDH)
- Hospitali ya Wilaya Mafinga
- Kituo cha Afya Usokami
- Kituo cha Afya Kasanga
- Hospitali ya Lugoda

***[Sikiliza radio ili kujua vituo vingine zaidi.]***

**Tohara ya Mwanaume**

***Maisha ni Sasa! Wahi Tohara!***
***Kuwa Msafi. Pata Kinga.***

**Wanaume wenye umri wa miaka 20 na kuendelea watapewa kipaumbele.**

**Kwa walio chini ya umri wa miaka 18 ni lazima waambatane na wazazi au walezi wao.**

Ili kujua zaidi kuhusu Tohara na faida zake tuma neno **TOHARA** kwenda **15014**
Ili kujua vituo vitoavyo huduma tuma neno **TABORA** au **IRINGA** kwenda **15014**

USAID KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI
Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii
MCHIP Maternal and Child Health Integrated Program
JOHNS HOPKINS BLOOMBERG SCHOOL of PUBLIC HEALTH
Center for Communication Programs
TANZANIANS AND AMERICANS IN PARTNERSHIP TO FIGHT HIV/AIDS

# KIPEPERUSHI CHA MWANAUME



**ni huduma BILA MALIPO**

**Tohara ya Mwanaume**

***Maisha ni Sasa! Wahi Tohara!***
***Kuwa Msafi. Pata Kinga.***

BFMMC2013


# **tohara**ya **mwanaume**

## Ukweli kuhusu tohara ya wanaume



Hii ni moja ya njia za zamani sana za upasuaji katika historia ya mwanadamu. Tohara hufanywa kwa sababu mbali mbali za kiutamaduni, kidini, kuboresha usafi na pia kwa sababu za kitabibu.

Hivi karibuni, watafiti wamegundua ya kwamba, tohara ya wanaume husaidia kupunguza hatari ya maambukizi ya VVU. Hii ni kwa sababu ngozi ya govi ni laini na rahisi kupata michubuko na vidonda na pia inazo chembe chembe hai maalumu ambazo huvutia virusi vya UKIMWI (VVU) kuingia mwilini kwa urahisi. Hivyo tohara husaidia kupunguza hatari hizi. Sasa, tohara inatolewa kwa wanaume wenye nia ya kupunguza uwezekano wa kupata VVU.



***Kwa muda wa wiki sita baada ya tohara, HUTAKIWI KABISA KUFANYA NGONO AU KUPIGA PUNYETO.***

Hii ni kwa sababu eneo lililofanyiwa upasuaji halijapona kikamilifu, hivyo unaweza kujitonesha au kujiingiza katika hatari zaidi ya kuambukizwa VVU.

Baada ya wiki sita kupita, ni muhimu kuendelea kuzingatia njia nyingine za kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU.



**Kuchukua uamuzi wa kufanyiwa tohara ni hatua ya muhimu katika maisha ya mwanaume.**

Tafadhali tembelea kituo cha afya kinachotoa huduma hizi kama vile hospitali ya mkoa, hospitali ya wilaya au kituo chochote cha afya ili uweze kufaidika na huduma hizi. Kwa maelezo zaidi kuhusu kituo kinachotoa huduma hizi kilichopo karibu na wewe, tuma ujumbe mfupi wa maandishi au [piga simu kwenda namba zilizotajwa nyuma ya kipeperushi hiki].

Tohara ya wanaume hupunguza hatari ya maambukizi ya VVU kwa kiwango cha hadi asilimia 60, kwa hiyo haiwezeshi kinga kwa asilimia 100. Hivyo basi wanaume waliotahiriwa bado wanahitaji kutumia njia nyingine za kujikinga na maambukizi ya VVU.

Tohara pia husaidia kujikinga dhidi ya baadhi ya magonjwa ya zinaa, maambukizi ya njia ya mkojo, na saratani ya uume. Wanaume wengi huelezea kuwa ni rahisi zaidi kujifanyia usafi baada ya tohara. Kama ilivyo kwa upasuaji mwingine wa aina yoyote, tohara ya wanaume inaweza kuambatana na matatizo madogo madogo kama kutokwa damu au jeraha na kupata maambukizi ya vijidudu kama bakteria.

Matatizo haya huweza kudhibitiwa kirahisi kwa kufuata vizuri maelekezo utakayopewa baada ya tohara, na pia kuwaona wahudumu wa afya pindi matatizo yanapojitokeza.



## Je,**tohara ya mwanaume inatoa kinga kamili dhidi ya maambukizi ya VVU?** Hapana.

Tohara ya wanaume katika kinga dhidi ya VVU inaweza kufananishwa na wachezaji katika mchezo wa mpira wa miguu. Wachezaji wengine ni pamoja na kutofanya ngono kabisa, kuwa na mwenzi mmoja mwaminifu aliyepima, kupunguza idadi ya wenzi na kutumia kondomu katika kila tendo la ngono.

Hawa ni kama walinzi wanaolinda goli na tohara ni golikipa ambaye ndio tegemeo la mwisho katika kulinda goli.

# Huduma ya tohara hutolewa katika hospitali ya mkoa, wilaya, na baadhi ya vituo vya afya.

**Kuna hatua kadhaa katika mchakato mzima wa kupatiwa huduma za tohara:**




**Hatua ya kwanza:**
Utashiriki katika ushauri nasaha wa kundi ili uweze kufahamishwa kuhusu faida na matatizo madogo madogo yanayohusiana na tohara na hivyo kukupa nafasi ya kufikia uamuzi iwapo unahitaji kupata huduma hii.




**Hatua ya pili:**
Utapewa ushauri nasaha binafsi ukiwa ana kwa ana na mhudumu wa afya mwenye ujuzi. Hapa utapata nafasi ya kumuuliza mhudumu maswali yoyote ya ziada uliyonayo na pia utapewa nafasi ya kupima VVU iwapo utaridhia. Pia, utafanyiwa uchunguzi wa afya yako ili kufahamu iwapo inafaa kukufanyia upasuaji.




**Hatua ya tatu**:
Utafanyiwa tohara na wahudumu wa afya wenye ujuzi. Tohara huchukua takribani dakika 30. Kabla ya upasuaji, utachomwa sindano ya ganzi panapostahili ili usipate maumivu wakati wa upasuaji. Baada ya tohara, kidonda kitafungwa vizuri kwa bandeji ili kukinga dhidi ya uambukizi wa vijidudu vya magonjwa.




**Hatua ya nne:**
Baada ya tohara, utapelekwa katika chumba cha mapumziko kabla ya kuruhusiwa kwenda nyumbani, pia utapewa dawa za kumeza ili kupunguza maumivu.

Baada ya kufanyiwa tohara ni muhimu upumzike kwa muda wa siku mbili. Hii ina maana usifanye kazi ngumu kama kubeba vitu vizito au kuendesha baiskeli. Unatakiwa kuvaa nguo zisizokubana ili kuepuka kujitonesha na kupata uambukizo wa vijidudu kwenye kidonda.

Baada ya siku mbili utatakiwa kurudi katika kituo cha afya ulichofanyiwa ili mhudumu aweze kutoa bandeji na pia kukagua kidonda chako. Vilevile unashauriwa kurudi katika kituo cha afya baada ya siku saba kwa uchunguzi na ushauri nasaha zaidi.

Pia, utapatiwa ushauri zaidi wa jinsi ya kukitunza kidonda chako baada ya tohara hususani katika kipindi cha wiki sita zinazofuata.

